Wakulima Wana Uwezo wa Kukomesha Kabisa Umaskini na Njaa, FAO Yasema

Na Friday Phiri

Dkt. Evelyn Nguleka, Rais wa Shirika la Kimataifa la Wakulima (WFO), akiwa na Katibu Mkuu Marco Marzano de Marinis. Picha ni kwa Hisani ya: Friday Phiri/IPS

LIVINGSTONE, Zambia, Mei 5 2016 (IPS) - Takwimu za hivi karibuni zinazoonyesha kwamba watu milioni 793 wanaenda kulala bila kula chakula, hii ndio changamoto kuu ya maendeleo duniani ambayo viongozi wa mataifa ya duniani wamelenga kukabiliana nayo katika miaka 15 na kukomesha kabisa njaa na umaskini.

Kama sehemu ya Malengo kumi na saba ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals-SDGs), masuala ya njaa na umaskini yamewekwa kama vipaumbele kulingana na athari zake kwa uwezo wa mataifa ya duniani kuafikia malengo mengine ya Maendeleo Endelevu.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) linafahamu uzito wa changamoto iliyopo ya kukabiliana na changamoto ya njaa na umaskini, na umuhimu wa wazalishaji chakula- wakiwemo wakulima, ili kutimiza lengo lililowekwa.

"Kama unavyofahamu, jamii ya kimataifa imejitolea kukomesha kabisa njaa na umaskini katika miaka 15, lengo linaloanadamana na uidhinishaji wa Ajenda ya Mwaka wa 2030. Shirika la Umoja wa Kimataifa la Chakula na Kilimo lina uwezo wa kushughulikia changamoto hizi. Lakini tunafahamu kwamba hili linawezekana tu kupitia ushirikiano thabiti, hasa ushirikiano baina ya washiriki wasio wa serikali, "Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Kimataifa la Chakula na Kilimo Bwana Graziano Da Silva, alisema haya wakati wa mkutano wa kimataifa wa Shirika la Kimataifa la Wakulima ambao ulifunguliwa hapa (jana) mnamo Jumatano, Mei 4.

Akizungumza na wajumbe katika mkutano huu kupitia ujumbe wa video, Da Silva alionyesha kwamba majukumu ya wakulima sio tu kuzalisha chakula lakini pia wana jukumu katika utunzaji wa mazingira, hii inatokana na madhara yanayotokana na mabadiliko ya hali ya anga yanavyoathiri Kilimo-Kisayansi, sekta ya kilimo inafahamika kama sekta inayoweza kuathirika pakubwa na mabadiliko hayo. "Wakulima wana wajibu wa kuzalisha chakula ambacho sisi sote tunakihitaji lakini pia wasaidie katika kuhifadhi na kuendeleza rasilimali zetu za asili."

Kama sehemu kubwa ya uwekezaji katika kilimo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo aliwahimiza wakulima kusaidiwa na kwamba, "wakulima wazingatiwe kama sehemu kuu ya mikakati ya uwekezaji wenye manufaa katika kilimo." De Silva akirejelea uhusiano wa Shirika la Kimataifa la Wakulima na mashirika mengine na umuhimu wake katika Miongozo ya Uwekezaji wenye Manufaa kwa Mifumo ya Kilimo na Chakula.

Miongozo hiyo iliyoandwaliwa na Jopo la Wataalamu la Inter -Agency Working Group (IAWG) liliondwa na Shirika la Umoja wa Kimataifa la Chakula na Kilimo, (FAO), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD), Halmashauri ya Kimataifa ya Ufadhili wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Benki ya Dunia, miongozo hii inachunguza haki na maisha ya za jamii zinazoishi katika sehemu za mashambani na haja ya kuwepo kwa uwekezaji wa kilimo endelevu kwa kijamii na kilimo kinachozingatia mazingira.

Miongozo hii inashughulikia kila aina ya uwekezaji katika kilimo, ikiwa ni pamoja na wawekezaji msingi na wakulima wa kimkataba. Kanuni hizi zinatokana na utafiti wa kina kuhusu mazingira, viwango na athari za uwekezaji wa sekta ya kibinafsi na mbinu bora katika sheria na sera. Miongozo hii inanuiwa kutoa mafunzo na kutoa mifumo ya udhibiti wa kitaifa, mikataba ya uwekezaji ya kimataifa, mikakati ya kushugulikia jamii ya makampuni na mikataba ya wawekezaji wa kibinafsi.

Wajumbe katika Shirika la Kimataifa la wakulima wamesisitizwa kwenye miongozo hii kama vifaa ambavyo vinaweza kutumika katika harakati za kushinikiza 'Ushirikiano wa Kukuza Uchumi', ambao ndio ujumbe mkuu wa Mkutano wa Kimataifa wa 2016.

"Mimi nina fahari ya kusema kwamba Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula na Shirika la Kimataifa la Wakulima wana uhusiano thabiti na wa kimkakati wa kuafikia usalama wa chakula na lishe bora na kilimo endelevu duniani kote. Pamoja na washiriki wengine, tumeboresha takwimu ili kuelewa jukumu la kiuchumi na la kijamii la mashirika ya wakulima katika maendeleo endelevu," Mkuu wa Shirika la Umoja wa Kimataifa la Chakula na Kilimo alisema.

Jukumu la Miongozo ya Hiari ya Uongozi wa Uwajibakaji wa Muda na wa Kudumu wa Kutumia Ardhi, Uvuvi na Misitu (VGGT), lina uhusiano wa karibu na uwajibikaji wa uwekezaji katika kilimo. Kama iliyoidhinishwa na Kamati ya Usalama wa Chakula Duniani mwaka wa 2012, miongozo hii inatumika kama marejeleo ya kuboresha muda wa kutumia ardhi wenye malengo makubwa ya kuafikia usalama wa chakula na kuunga mkono utambuzi wa kimaendeleo wa haki ya kupata chakula cha kutosha kwa wote.

Hii ilitokana na utambuzi kwamba muda wa kuitumia ardhi ungali unadhibitiwa na serikali na hii ni miongoni mwa changamoto muhimu ambazo wakulima wanakumbana nazo, hasa katika mataifa yanayoendelea. Kimsingi, wakulima wadogo, hasa wanawake, wanalima ardhi ambayo hawamiliki, hali hii imezalisha umaskini zaidi uliokithiri unaowakumba wanawake na ukosefu wa nguvu za kisiasa.

Kutokana na matamshi ya Waziri wa Kilimo wa Zambia kuwa "Barani Afrika ndiko kuna idadi kubwa ya wakulima wadogo ambao huzalisha mali, na kuilisha dunia", vipengele vya kupata ardhi, kuimiliki na kuidhibiti na kutumia teknolojia ya kisasa, kupata masoko na rasilimali za kifedha, ni

vigezo muhimu ili kuwawezesha wakulima wadogo kuboresha ufanisi na uzalishji katika kilimo.

Katika kuongeza msukumo wa usalama wa kutumia ardhi na chakula kama kipengele muhimu katika uafikiaji wa Malengo ya Mandeleo Endelevu, Mwenyekiti wa Kamati ya Umoja wa Kimataifa ya Usalama wa Chakula (Committee on World Food Security -CFS), Balozi Amira Gornass alisema "Wakulima ndio uti wa mgongo wa hatua zozote za kuafikia usalama wa chakula na lishe bora..."

Balozi Gornass anaamini kwamba "Maendeleo endelevu kwa wote yanawezekana" kupitia ushirikiano na washiriki wote wa uzalishaji chakula ili kuhakikisa kwamba kufikia mwaka wa 2030 "tutaangamiza kabisa njaa na hakuna anayesalia katika hali ya njaa."

Akilenga zaidi ujumbe mkuu wa mkutano huu wa kimataifa, Rais wa Shirika la Kimataifa la Wakulima Evelyn Nguleka, alisema kwamba jukumu la kilimo na wakulima katika kukabiliana na baadhi ya malengo yaliyowekwa na ajenda mpya ni muhimu, kwa kuwa unajumuisha baadhi ya malengo yalioyopendekezwa.

"Uchumi wa dunia unategemea zaidi vigezo vya utendakazi na faida. Wakulima, kama wajasiriamali wengine wowote, wanahitaji kuona kazi yao ikifidiwa na mapato yafaayo na bidhaa zao zikitumika katika soko la wanunuzi ifaavyo. Wakulima wapo tayari kuwekeza siku zao katika mashamba, huku wakitafuta suluhisho mpya ili kuongeza faida zinazotokana na mashamba yao.., "Gornass alisema.

(Mwisho)